## HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI
## MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI CHA TAREHE 31/05/2024
## KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA COMMUNITY CENTRE

**MAHUDHURIO**

**A. WAJUMBE**

| NA. | JINA | | CHEO | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Pancras | Maliyatabu | -Mwenyekiti wa Halmashauri | **-Mwenyekiti** |
| 2. | William | Mwakalambile | -Mkurugenzi Mtendaji (W) | **-Katibu** |
| 3. | Mhe. Stephen | Kayogolo | -Makamu Mwenyekiti H/W | -Mjumbe |
| 4. | Mhe. Egid | Ngomeni | -Diwani Kata ya Nkomolo | -Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mpemba | Evarist | - Diwani Kata ya Nkandasi | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dismas | Msangawale | -Diwani Kata ya Kate | -Mjumbe |
| 7. | Mhe. Badwin | Mathew | -Diwani Kata ya Mashete | -Mjumbe |
| 8. | Mhe. Maria | Ndauka | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Namanyere | -Mjumbe |
| 9. | Mhe. Osward | Kamsipi | -Diwani Kata ya Kizumbi | -Mjumbe |
| 10. | Mhe. Asante | Lubinsha | -Diwani Kata ya Kabwe | -Mjumbe |
| 11. | Mhe. Muhamad | Zaid | -Diwani Kata ya Mkinga | -Mjumbe |
| 12. | Mhe. Vitalis | Malipesa | -Diwani Kata ya Korongwe | -Mjumbe |
| 13. | Mhe. Janeth | Kashamakula | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | -Mjumbe |
| 14. | Mhe. Emiliana | Kauzeni | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kate | -Mjumbe |
| 15. | Mhe. Magreth | Maembe | -Diwani Viti Maalum Tarafa yaNamanyere | -Mjumbe |
| 16. | Mhe. Wensensilaus | Kapita | -Diwani Kata ya Ninde | -Mjumbe |
| 17. | Mhe. Robert | Kasongo | -Diwani Kata ya Mkwamba | -Mjumbe |
| 18. | Mhe. Nestory | Kaloto | -Diwani Kata ya Namanyere | -Mjumbe |
| 19. | Mhe. Godfrid | Bendera | -Diwani Kata ya Majengo | -Mjumbe |
| 20. | Mhe. Garincha | Kiliko | -Diwani Kata ya Itete | -Mjumbe |
| 21. | Mhe. Joseph | Mwenda | -Diwani Kata ya Kipande | -Mjumbe |
| 22. | Mhe. Francis | Nkoswe | -Diwani Kata ya Ntuchi | -Mjumbe |
| 23. | Mhe. Kakuli | Seba | -Diwani Kata ya Kirando | -Mjumbe |
| 24. | Mhe. Mohamed | Adam | -Diwani Kata ya Kipili | -Mjumbe |
| 25. | Mhe. Frank | Mtakwita | -Diwani Kata ya Wapembe | -Mjumbe |
| 26. | Mhe. Gerald | Kalikisha | -Diwani Kata ya Sintali | -Mjumbe |
| 27. | Mhe. Karolina | Makandi | -Diwani Kata ya Paramawe | -Mjumbe |
| 28. | Mhe. George | Saninga | -Diwani Kata ya Myula | -Mjumbe |
| 29. | Mhe. Roswita | Sululu | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | -Mjumbe |
| 30. | Mhe. Ruteghata | Miambi | -Diwani Viti Maalum Tara ya Chala | -Mjumbe |
| 31. | Mhe. Kudra | Ahamed | -Diwani Kata ya Kipundu | -Mjumbe |
| 32. | Mhe. Isaack | Chambula | -Diwani Kata ya Isunta | -Mjumbe |
| 33. | Mhe. Masai | Leonard | -Diwani Kata ya Ntatumbika | -Mjumbe |
| 34. | Mhe. Privatus | Yolam | -Diwani Kata ya Kala | -Mjumbe |
| 35. | Mhe. Michael | Mwanalinze | -Diwani Kata ya Chala | -Mjumbe |
| 36. | Mhe. Anastazia | Kasagama | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kirando | -Mjumbe |
| 37. | Mhe. Priska | Mbeyu | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Chala | -Mjumbe |
| 38. | Mhe. Aida | Khenani | -Mbunge Nkasi Kaskazini | -Mjumbe |

HUDHURIA

Mhe. Vicent Mbogo (MB) -Mjumbe- -Kwa Taarifa

**B. WATAALAM**

| NA. | JINA | | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Nsubisi | Mwakasege | Kaimu Afisa Utawala na Utumishi (W) |
| 2. | Dafrosa | Mkenda | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 3. | Lucia | Mwani | KaimuAfisa Maendeleo ya Jamii(W) |
| 4. | Opotunas | Mussi | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 5. | Dr John | Tlatlaa | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 6. | Alinutwa | Nkundwe | Kaimu Afisa Ugavi na Manunuzi (W) |
| 7. | Akimu | Danda | Kaimu Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W) |
| 8. | Consolata | Mwingira | Kaimu Afisa Mazingira na Udhibiti TakNgumu (W) |
| 9. | Charles | Kisanga | Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Mamlaka Mji Mdogo Namanyere |
| 10. | Salu | Makoye | Kaimu Mkaguzi wa Ndani |
| 11. | Christopha | Lameck | Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 12. | Ladslaus | Mzelela | Afisa Kilimo, Takwimu na Ufuatiliaji (W) |
| 13. | Valeriana | Mwapasi | Afisa Mali asili na Utunzaji Mazingira |
| 14. | Erick | Kilimo | Kaimu Mweka Hazina |
| 15. | Ghambi | Idon | Kaimu Afisa Uchaguzi (W) |
| 16. | Richard | Katyega | Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu (W |
| 17. | Osward | Msengezi | Kaimu Afisa Ardhi na Mali asili (W) |
| 18. | Godfrey | Segenge | Kaimu Mhandisi Wa Ujenzi |
| 19. | Emmanuel | Tinga | Kaimu Mwanasheri wa Halmashauri |
| 20. | John | Ntulo | Kaimu Afisa TEHAMA (W |
| 21. | Patrick | Kipesha | Mwandishi wa Vikao |

**C. KAMATI YA ULINZI NA USALAMA**

| NA. | JINA | | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Peter | Lijualikali | Mkuu wa Wilaya- Nkasi |
| 2. | Samweli | Kiswaga | -Kaimu Afisa Usalama (W) |
| 3. | Elisante | Tumbo | -Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| 4. | Insp Atupele | Mwakaliku | -Kaimu Mkuu wa Jeshi la Polisi -Nkasi(W) |
| 5. | CPL Syprian | Mhuvi | -Kaimu DFO |
| 6. | Mj BW | Peter | -Mshauri wa Mgambo (W) |
| 7. | CPL Shadrack | Sambo | -Mkuu wa kikosi cha Akiba Namanyere |
| 8. | Joseph | Mabula | -Kaimu Mkuu DBC |
| 9. | IC Safiel | John | -Kaimu DIO |

**D. MAAFISA TARAFA**

| NA. | JINA | | CHEO | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Diana | Khan | -Afisa Tarafa | Chala |
| 2. | Kasimu. | Ibrahim | -Afisa Tarafa | Namanyere |
| 3. | Revocatus | Chikala | -Kaimu Afisa Tarafa | Kirando |
| 4. | Frasto. | Widambe | -Kaimu Afisa Tarafa | Wampembe |

Revocatus Chikala -Kaimu Afisa Tarafa Kate

E. **WAGENI WAALIKWA**

| NA | JINA | | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Lumara | Madirisha | Kaimu Meneja TARURA(W) |
| 2. | Marya | Nsongo | Kaimu Meneja Ruwasa (W) |
| 3. | Thomas | Petro | Kaimu Meneja Ruwasa(W) |
| 4. | Vitalis | Lyela | M/KitI Shidepha |
| 5. | Kamilius | Nguruwe | M/kiti Mamlaka ya Mji Mdogo Namanye |

- **WAANDISHI WA HABARI**

| NA. | JINA | | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Israel | Mwaisaka | - Mtangazaji Nkasi FM |
| 2. | Pety | Siame | -Mwandishi wa Habari TBC |
| 3. | Guriano | Adolf | -Mwandishi wa Habari Nipashe |
| 4. | Baraka Lusajo | | -Mwandishi wa Habari ITV |

## AGENDA.NA.NKS/DC/BRZ/01/06/2024
## KUFUNGUA KIKAO

tibu wa kikao aliwakaribisha wajumbe wataalam, wageni waalikwa, na wananchi waliohudhuri raza, kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufungua kikao.

wenyekiti wa kikao alifungua kikao mnamo saa 5:45 asubuhi na aliwasihi wajumbe kuwasilish arifa kwa ufupi na kuzingatia kanuni za uendeshaji wa vikao.

## AGENDA.NA.NKS/DC/ BRZ /02/06/2024
## KUTHIBISHA AGENDA

ajumbe walithibitisha agenda

## AGENDA.NA.NKS/DC/ BRZ /03/06/2024
## KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA

wenyekiti wa kikao aliwapitisha wajumbe ukurasa kwa ukurasa wa muhtasari na kufany rekebisho. Wajumbe waliridhia muhtasari usainiwe kama kumbukumbu ya nyaraka za Halmashauri ada ya hapo Katibu alikaribisha Taasisi zilizojiandaa kuwasilisha mada kwa Waheshimiwa Madiwan ma ifuatavyo;

A. TARURA

Kaimu Meneja wa TARURA aliwasilisha taarifa ya kazi zilizofanyika katika kipindi cha robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024.Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo

-Wajumbe walihoji suala la barabara za vijijini zitatengenezwa lini maana kwa sasa muda wa kusafirisha mazao umefika hivyo ni muhimu sana barabara hizo kufunguliwa

-Mjumbe mwingine alihoji suala la vifusi vilivyowekwa katika barabara toka Halmashauri kwenda kwa Mkuu wa Wilaya vitasambazwa lini

Baada ya michango ya wajumbe Kaimu Meneja RUWASA alifafanua kuwa barabara zinaendelea kufunguliwa kwa kuwatafuta wakandarasi ili kufanya kazi hizo suala la vifusi vilivyopo katika barabara toka Halmashauri kwenda Ikulu Meneja ameenda kulifuatilia Wajumbe waliunga mkono hoja

B. RUWASA

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya maji aliwasilisha taarifa ya kazi zilizofanyika katika kipindi cha robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

-Mjumbe alipongeza chama cha Mapinduzi kwa kuhakikisha maji yanapatikana katika kata ya Isale hivyo ombi yasambazwe katika nyumba za Wananchi

-Mjumbe alihoji juu ya mabomba yaliyopo kata ya Kirando kuwa Mkandarasi aliyekuwa akitekeleza mradi huo siku za nyuma aliyaleta na aliyaacha na kwa sasa akiuliza kuwa ni ya nani anasema ni yak wake kimsingi wananchi wanajua ni mali ya Serikali hili suala likoje

Kaimu Meneja RUWASA alipokea pongezi na kufafanua kuwa mabomba yale ni ya Serikali na Mkandarasi anatakiwa kuyakabidhi. Wajumbe walipokea ufafanuzi na kuunga mkono hoja

AGENDA. NA.NKS/DC/ BRZ /04/06/2024

**UPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA KATA ROBO YA TATU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

ajumbe waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Kata ambapo taarifa za Kata zifuatazo ziliwasilishwa; Kata ya *Chala, Isale, Ntuchi, Isunta, Itete, Kabwe, Kala, Kate, Kipande, Kipili, Kipundu, Kirando, Kizumbi, Korongwe, Majengo, Mashete, Mkinga, Mkwamba, Mtenga, Myula, Namanyere, Ninde, Nkandasi, Nkomolo, Ntatumbila, Paramawe, Sintali* na *Wampembe.* Baada ya kuwasilisha taarifa wajumbe walipata nafasi ya kuchangia kama ifuatavyo: -

- Mjumbe aliashauri asilimia 10 za Vijiji zirudishwe kwa wakati ili kusaidia katika shughuli za maendeleo
- Mjumbe alipongeza Mkurugenzi Mtendaji kwa kusimamia vizuri suala la mapato na kuomba juhudi kuongezeka ili kufikia asilimia zilizopangwa
- Wajumbe walishauri kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ununuzi wa Mashine za kukusanyia Mapato (POS Mashine) liwe jambo la kipaumbele ili kuhakikisha vituo vyote vinakuwa na mashine hizo.
- Mjumbe aliomba ufafanuzi kuhusiana na utengenezaji wa choo cha stendi kwani kinakosesha watumiaji raha na ni hatari kwa maisha yao
- Mjumbe alitaka kujua sababu zilizopelekea kuvunja kwa mkataba wa Mkandarasi katika shule mpya ya Sekondari Kizumbi
- Wajumbe walishauri ili kuweza kufikia lengo katika ukusanyaji wa mapato hasa ukanda wa ziwa Tanganyika Mkurugenzi Mtendaji aweke mikakati mathubuti kwani mapato yapo ya kutosha
- Mjumbe alishauri Watendaji wanaokusanya mapato vizuri waweze kupewa motisha ili kuendelea kuwapa moyo katika kuchapa kazi
- Mjumbe mwingine alishauri matumizi ya fedha za Halmashauri yatumiwe vizuri ili kuweza kupata fedha za kufanya maendeleo kwa Wananchi
- Ushauri mwingine ulikuwa ni kuchukua hatua za haraka kwa wale wote wanaofanya juhudi za kutorosha mapato ya Halmashauri

Baada ya hoja za wajumbe Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwapongeza wajumbe kwa kuwasilisha taarifa za kata, pia alipokea ushauri na kuahidi yote yaliyoshauriwa yatafanyiwa kazi

AGENDA. NA.NKS/DC/ BRZ /05/06/2024

**KUFUNGA KIKAO**

Katibu wa kikao aliwapongeza wajumbe kwa michango yenye tija kwa maendeleo ya Halmashauri, na alipokea ushauri uliotolewa na kuahidi maagizo na maelekezo yatazingatiwa, kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga kikao

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa uwasilishaji wa taarifa pamoja na maoni yao, pia alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji (W) pamoja na Wakuu wa Idara na vitengo kwa ufafanuzi na akasisitiza maagizo yaliyotolewa yatekelezwe.

Kikao kilifungwa saa 7:15 mchana

MUHTASARI UMETHIBITISHWA/HAUJATHIBITISHWA

| | |
|---|---|
| ………………………………… | ………………………………… |
| WILLIAM MWAKALAMBILE | MHE.PANCRAS MALIYATAB |
| KATIBU | MWENYEKITI |

Tarehe